

Ubadilishaji Msimbo kama Mbinu ya Upole Chana katika Vipindi vya *Sobetab Kapchi* kwenye Idhaa ya KASS FM

Muge Tecla
Chuo Kikuu cha Moi, Kenya

Ikisiri

Makala haya yanahusu nafasi ya ubadilishaji msimbo kama mbinu ya upole katika vipindi vya *Sobetab Kapchi* (SK) katika idhaa ya KASS FM. Utafiti uliongozwa na maswali mawili: je, wahusika katika vipindi vya SK wanachopeka maneno ya Kiswahili kwenye mazungumzo yao? Je, huku kubadilisha msimbo kunatokea katika hali zipi? Aidha, utafiti ulielekezwa na Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987), hasa kipengele cha kuokoa uso. Vipindi vinne vya mazungumzo ya SK vilinaswa. Data zilizohusiana na upole kutoka kwa vipindi husika zilinakiliwa na kuchanganuliwa. Baadhi ya data zilinukuliwa moja kwa moja na zingine zilifupishwa kutegemea urefu wa data. Ilibainika kuwa, wasemaji wa Kinandi katika mazungumzo ya SK huchopeka maneno ya Kiswahili kwenye mazungumzo yao. Aidha, UM hutokea wakati wasemaji wanafikiria kuwa neno la Kinandi linaweza kutishia nyuso za wahusika wa mazungumzo.

Maneno Makuu: Upole Chanya, Upole Hasi, Kuokoa Uso, Sobetab Kapchi, KASS FM

Utangulizi na Mapitio ya Maandishi

Kazi hii ni uchanganuzi wa athari ya lugha ya Kiswahili katika Kinandi. Ni uchanganuzi wa uamilifu wa ubadilishaji msimbo (UM) katika mazungumzo ya *Sobetab Kapchi* (Maisha ya jamii) katika idhaa ya KASS FM. Hususan, mazungumzo husika yamejikita katika UM kama njia mojawapo ya kutekeleza upole chanya. Ni uchanganuzi wa jinsi wahusika wa vipindi vya *Sobetab Kapchi* (SK) wanachopeka maneno ya Kiswahili katika mazungumzo yao ya Kinandi. Uchopekaji huo hutokea kama njia ya kurahisisha mawasiliano kupitia kwa lugha ya ustaarabu au upole.

Lugha ni zana inayotumika kukuza uhusiano baina ya watu. Wakati wa kuwasiliana, watu huchagua mbinu zitakazowawezesha kupatana. Washiriki wa mazungumzo hutumia mikakati ya upole kuhakikisha kuwa mawasiliano

yanafanyika bila mkwaruzano. Kuwa mpole hakumhitaji mtu kujua lugha tu bali pia kuelewa kaida na tamaduni zinazothaminiwa na jamii husika. Kwa ujumla, kuwa mpole ni kujali hisia za wengine kwa kuhakikisha kuwa wanastareheka

Kila jamii-lugha huwa na kanuni maalum ambazo hutawala mazungumzo yoyote yale. Kanuni hizo huwezesha mawasiliano na maelewano baina ya wazungumzaji na pia kuboresha mahusiano baina yao. Kanuni mbalimbali kama vile kuzungumza kwa sauti, kubadilishana zamu na vilevile kuwa makini hutawala mazungumzo yoyote. Brown na Levinson (1978, 1987), wanaeleza kuwa mazungumzo yoyote yale huwa tishio kwa nyuso za wahusika, na mazungumzo katika vipindi vya (SK) hayaepuki ukweli huu.

Mazungumzo katika Vyombo vya Habari

Mazungumzo katika vyombo vya habari hujadili mada nyingi zinazovutia na kwamba uchanganuzi wa upole ni moja tu ya mada hizo (Petrickova, 2012). Kuna sababu nyingi ambazo kwazo mawasiliano katika vyombo vya habari yanafaa kuchanganuliwa katika mtazamo wa upole. Mawasiliano katika vyombo vya habari huashiria muundo wa mazungumzo ambao hutawaliwa na kanuni nyingi za mazungumzo rasmi. Vilevile, kulingana na Petrickova (2012, uhusiano tata baina ya makundi yanayoshiriki mazungumzo hayo huashiria umuhimu wa uteuzi makinifu wa mikakati ya upole katika mazungumzo yoyote.

Vipindi vya redio ni njia mojawapo ya kufahamisha umma kuhusu masuala tofauti ya kisiasa, kijamii, na kiuchumi. Vipindi hivi huwa ama vimerekodiwa awali kabla ya kupeperushwa hewani au hupeperushwa hewani moja kwa moja wakati wa mahojiano. Wanahabari huwaalika wataalamu mbalimbali wenye tajriba kuhusiana na mada tofautitofauti ili kuwahusisha katika mijadala ya kuwafahamisha wanajamii kuhusu matatizo yanayowakumba na namna ya kukabiliana na matatizo hayo.

Nchini Kenya, kuna vituo vya redio vinavyopeperusha vipindi kupitia lugha rasmi; Kiswahili na Kiingereza. Baadhi ya vituo hivyo ni *Citizen*, *Kiss FM*, *RadioMaisha*, na *BBC*. Kuna vituo vinavyorusha matangazo kwa lugha za mama. Vituo hivyo ni pamoja na *MusiFM* (Kikamba), *KassFM* (Kikalenjin), *InooroFM* (Kikuyu), *Chamgei FM* (Kikalenjin), *Ramogi FM* (Kijaluo), *KitwekFM* (Kikalenjin), *Sulwe FM* (Kiluhya), *IngoFM* (Kiluhya) miongoni mwa vituo vingine. Vituo hivi hupeperusha vipindi mbalimbali vya mazungumzo kupitia mahojiano na viongozi, wasanii na wataalamu mbalimbali.

KASS FM ni kituo cha kibinafsi nchini Kenya ambacho hutumia Kikalenjin. *Kass*ni neno linalotumiwa na lahaja zote za Kikalenjin kwa maana ya 'sikia' na kwa hivyo hutumiwa katika idhaa hii kurejelea kituo kinachosikilizwa na wasemaji wa Kikalenjin. Kulingana na www.kassfm.co.ke, vipindi vya *Kass* husikilizwa na zaidi ya asilimia tisini na mbili (92%) ya Wakalenjin wa Kenya kando na

wasikilizaji Wakalenjin wa nchi jirani kama vile Tanzania, Uganda, Rwanda, Burundi na Sudan Kusini. Isitoshe, baadhi ya Wakalenjin wanaoishi ughaibuni husikiza kituo hiki na mara nyingi huchangia katika mada husika.

Kituo cha redio cha Kass kina vipindi anuwai kama vile *Kwondo ne Ng'om* (mke mwenye hekima), *Len Nee Emet?* (Kuna nini nchini?), *Teeb si Inai* (Uliza ujibiwe), *Twoliot* (Mambo ya ngono), *TigitiotabBambaniat* (Chanzo cha mapenzi) na kipindi kimojawapo maarufu ni *Sobetab Kapchi* (Maisha ya jamii). *Sobetab Kapchi* (SK) huwasilishwa kila Jumatano saa nne hadi saa sita usiku. Kwa mujibu wa www.kassfm.co.ke, kipindi hiki kina mashabiki wengi kutokana na mada zake ambazo huwajaza wasikilizaji mengi kuhusiana na masuala ya kijamii hasa katika asasi ya ndoa. Kipindi hiki huangazia masuala kama vile malezi bora, mpango wa kando, uke wenza, ukosefu wa uaminifu katika ndoa, talaka, mahusiano na mashemeji na jinsi ya kukabiliana na changamoto hizo.

Umaarufu wa kipindi hiki hutokana na sababu kwamba wasikilizaji hupewa fursa ya kuchangia kwa kuuliza maswali au kutoa maoni yao. Kupitia kwa kipindi hiki, wasemaji wa Kikalenjin hupata sio tu ufahamu kuhusu masuala tofauti katika jamii bali hata burudani. Aidha, mwasilishaji mkuu wa kipindi pamoja na mwelekezi wa kipindi wana namna ya pekee ya kuwasiliana na wasikilizaji wao ili wapate kuelewana nao.

Mazungumzo katika vipindi hivi vya SK huhitaji upole kwa sababu hujadili masuala muhimu ambayo mara nyingi huhitaji umakinifu wa wahusika. Katika mazungumzo mbalimbali, wazungumzaji huhitajika kutumia mbinu mbalimbali za upole ili kuhifadhi nyuso zao na za wasikilizaji wao. Ni kwa msingi huo ndipo makala haya yanachambua ujipenyezaji wa maneno ya Kiswahili kwa Kinandi kama mbinu mojawapo ya upole.

Katika mazungumzo ya vipindi vya SK, mwasilishaji mkuu (Rotich) ana tajriba pevu katika mambo yanayohusiana na ndoa. Kwa muda mrefu, Rotich amefanya ushauri kanisani, katika mikutano ya akina mama, katika mikusanyiko ya wazee na pia katika mikutano ya vijana. Uzoefu huu wa kushauri, kuonya na kutoa mwelekeo umemfanya kujulikana kupewa kama 'Pasta'. Kwa kweli Rotich si kasisiwa dhehebu lolote lakini kazi anayoifanya na namna anayoifanya imempa sifa nyingi mno. Pamoja naye ni mwelekezi wa kipindi Winny Jepkorir ambaye huwaandaa mashabiki wa kipindi kupitia ucheshi wake. Wakati mwingine, jina Jepkorir linafupishwa na kutajwa kiutani kama 'Koriryo'.

Upole katika Utamaduni wa Wanandi

Kulingana na Wakalenjin hasa Wanandi, upole ni kuenenda kulingana na matakwa ya jamii. Mwanajamii ataonekana mpole iwapo atafanya kinachokubalika machoni mwa wenzake. Watu hufunika nyuso zao wanaposikia neno linaloteta aibu. Kulingana na Wakalenjin waliohojiwa, kuficha uso hutokana na uwezekano kuwa

neni limesemwa kwa njia isiyo faa. Kule kufunika kwa uso kunamaanisha kuwa msememwa amemwa haya kwa sababu kilichosemwa ni kinyume na matarajio yake.

Dhana ya uso ni muhimu sana katika utamaduni wa Wanandi. Wao huzingatia na kujali sana jinsi wanajamii wengine wanawachukulia. Dhana *keuny togoch* (kuficha uso) hutumika kurejelea hali ambayo watu hujipata baada ya kufanya, kusema au kufanyiwa kile ambacho ni kinyume na matarajio ya jamii husika. Kwa mfano, mtu huogopa kumkemea mwenzake hadharani kwa sababu miongoni mwa Wanandi huko ni kukosa adabu. Mtu anayependa kusema mambo ovyo bila kujali nyuso za wengine mara nyingi hupewa lakabu *yaach ng'ala* (mwenye maneno machafu).

Wanandi hupenda ustaarabu. Kwao, kustaarabika ni kutomkasirisha au kutomfanya mwingine ahisi vibaya. Miongoni mwa Wakalenjin, mja aliyestaarabika huchukuliwa kuwa mpole. Kama jamii zingine za Kiafrika, Wanandi huzingatia mikakati fulani katika mazungumzo ili kuokoa nyuso za wahusika katika mazungumzo. Baadhi ya mikakati hiyo ni: kusema neno kimzunguko, kutumia tasfida, kutosema kabisa jambo linalotishia uso, maswali ya balagha na ubadilishaji msimbo ambao ndio nguzo wa mjadala wetu. Kama wasemavyo Allan na Burrige (2006), kuna maneno ambayo kila jamii huyachukulia kuwa mwiko kuyataja. Jamii ya Wakalenjin ina maneno mengi ambayo yakitajwa hadharani, hutishia nyuso za washiriki wa mazungumzo. Hiyo ndiyo sababu ubadilishaji msimbo hutumika kupunguza makali ya maneno hayo.

Ubadilishaji Msimbo kama Mbinu ya Upole

Kama matokeo ya mtagusano wa lugha katika jamii, ubadilishaji msimbo (UM) unaelekea kuwa mada muhimu. Kama mojawapo ya mbinu za upole chanya, UM umekuwa nguzo katika tafiti nyingi zinazohusiana na upole. Upole ni dhahirisho la tamani la msemaji kupunguza vitisho fulani kwa uso wa mtu mwingine (Watts 2003, Mills 2003). Brown na Levinson (1987) wanaeleza upole kama namna ya kuokoa uso wa msikilizaji. Kijumla, upole ni hulka ya kiasili ya tabia njema na ni dhana ya kiakili na kijamii ambayo hukuzwa kupitia mahusiano yetu ya kijamii. Njia mojawapo ya kutekeleza upole ni UM. UM ni matumizi ya lugha mbili au zaidi katika mazungumzo. Ni hali ya kutumia zaidi ya launi moja katika mazungumzo (Myers-Scotton 1993, Djoko 2006). Watu hubadilisha msimbo wakati wa mazungumzo kwa nia moja au nyingine mojawapo ikiwa kukwepa kutaja mambo ya aibu katika lugha zao. Baadhi ya wale wanaotumia UM kama ukwepaji wa kutaja mambo bayana ni wahusika wa mazungumzo ya redio katika vipindi vya *SK* katika idhaa ya *KASS FM*.

Kwa kipindi kirefu sasa, wataalamu wengi wameshughulikia masuala ya upole. Mengi yamechunguzwa kuhusiana na upole katika riwaya, tamthilia na vipindi vya runinga lakini machache yamefanywa kuhusiana na upole katika mazungumzo. Bailey (2001) anaangalia majukumu ya kijamii ya kuchanganya msimbo miongoni

mwa wana Dominiko wa Kimarekani. Alichunguza UM katika kiwango cha wanafunzi wa shule ya sekondari na akapata kuwa wana Dominiko wa Kiamerika hubadili msimbo ili kufaidi mazungumzo yao ya kila siku baina yao wenyewe. Uchunguzi huo ni faafu sana kwa sababu unabainisha athari za UM sambamba na utafiti wa uchunguzi wa SK katika redio ya Kass FM. Muthuri (2000) anaangalia majukumu ya kubadili msimbo miongoni mwa wanafunzi wenye wingi-lugha katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Anagundua kuwa wanafunzi hao hubadilisha msimbo wanapozungumzia mambo yao ya kisiri.

Uchunguzi mwingine ni wa Kanana (2003) ambaye ameangalia matumizi ya msimbo katika soko moja la 'Village Market' jijini Nairobi. Aligundua kuwa wauzaji kwa wanunuzi hubadili msimbo ili kurahisisha mawasiliano yao ya kibiashara. Kuna baadhi ya maneno ambayo yakisemwa kwa lugha ya kiasili, hutishia nyuso za wahusika wa mazungumzo. Vipindi vya SK kinashuhudia ukweli huu kwa sababu wasemaji wameonekana kukwepa maneno ya lugha yao na badala yake wanatumia Kiswahili ili kurahisisha mawasiliano. Hii ni dhahirisho kuwa lugha ni chombo muhimu kinacholeta ushirikiano katika jamii na hutumiwa na wanajamii kujieleza.

Ogechi (2002) alitafitia na kuandikia kuhusu UM miongoni mwa jamii ya Abagusii, matokeo ya utafiti wake yanaonyesha kuwa UM hutumiwa wakati mwingine kama mbinu ya kuficha siri hasa miongoni mwa wanafunzi ambao ni wachumba. Utofauti huu humwelekeza mwasilishaji mkuu na mwelekezi wa vipindi kutumia lugha ya heshima wakati wa mjadala kama njia ya kujali uso wa hadhira. Baadaye, Ogechi (2002) Alichunguza UM miongoni mwa wazungumzaji wa Ekegusii na matumizi ya Sheng nchini Kenya. Alitoa maelezo ya kina kuhusu tofauti kati ya UM, uchanganyishaji msimbo na uhamishaji msimbo. Anaeleza kuwa, UM unasababishwa na ujuzi wa lugha hasa miongoni mwa washiriki wa mazungumzo walio na umilisi wa lugha zaidi ya moja yaani uwingi-lugha.

Kazi hii iliongozwa na nadharia ya upole, hasa mhimili wa kuokoa uso, kama inavyopendekezwa na Brown na Levinson (1987). Nadharia ya upole ina msingi wake katika kaida nne za kanuni ushirika ya Grice (1975). Kama mbinu mojawapo ya mikakati ya upole, Brown na Levinson (1987) wanaigawa mkakati wa kuokoa uso katika sehemu mbili: uokoaji wa uso chanya na uokoaji wa uso hasi. Kwa mtazamo wa nadharia hii, dhana ya uso inaweza kugawanywa katika sehemu mbili: uso chanya na uso hasi. Uso chanya ni hali ya mshiriki wa mazungumzo kutamani hisia zake zikubalike na wenzake katika mawasiliano; nao uso hasi ni hali ambayo kwayo mtu hataki kuzuiliwa kuzungumza anavyotaka.

Nadharia ya upole inapendekeza kuwa wakati wa kuwasilisha ujumbe, msemaji anafaa kuzingatia sana hisia za msikilizaji na vilevile aweze kupitisha ujumbe bila kuzua utata. Hapa ndipo panapatikana muumanao kati ya nadharia ya upole na kanuni ushirika. Grice (1975) anaigawa kanuni ushirika katika kaida nne ambazo ni

kaida za: kiasi, ubora, uhusiano na namna. Kwa ujumla, kanuni ushirika inasisitiza kwamba, msemaji anafaa kufanya mchango wake kwanja inayofaa na katika mwelekeo unaokubalika katika mazungumzo anayoshiriki. Nadharia ya upole basi, imetumika kuhakiki UM kama mbinu ya upole katika mazungumzo ya vipindi vya SK kwenye idhaa ya *KASS FM*.

Utafiti huu ulikuwa wa nyanjani. Utafiti ulitumia mbinu ya uchunguzi kistahilifu kwa sababu data iliyokusanywa ni matamshi ya wahusika katika vipindi teule na kwamba sehemu kubwa ya utafiti huu ni maelezo ya mbinu zilizotumika kufanikisha kipindi cha SK. Aidha, kwa kuwa utafiti ni wa kistahilifu, mchakato wa uchunguzi ulikuwa wa kiduara. Yaani, baada ya kumaliza hatua moja, kulikuwa na uwezekano wa kurudi katika hatua zilizotangulia ili kubadilisha vipengele vingine kwa minajili ya kuboresha kazi.

Uchanganuzi na Ufasiri wa Data

Wakati mwingine, ni vigumu kwa watu kutaja maneno fulani katika lugha yao. Hii inatokana nasababu kuwamaneno kama hayo huonekana kuwakosesha heshima. Wazungumzaji hujipata katika hali ya kupenyeza maneno ya lugha nyingine ndani ya lugha yao. Hii ni kwa kuwa, UM huja kama njia ya kipekee ya kumsaidia mtu kama huyo kufanikisha mawasiliano yake. Myers-Scotton (1993) anatoa dhana ya ubadilishaji msimbo kama hali ya kutumia zaidi ya lugha moja katika mazungumzo. Holmes (2001) anasema kuwa UM hutokea katika aina mbili:

1. UM unaotokea kulingana na wakati au na muktadha (kitasfida)
2. UM unaotokea kimapumbo.

UM Kiwakati, Kimuktadha au Kitasfida

UM kiwakati hufanyika wakati ambapo msemaji anataka kuweka ujumbe wake wazi kwa msikilizaji ili ueleweke vyema. Hutokea wakati msemaji anahisi kuwa lugha anayotumia haiwezi kumwezesha msikilizaji kuupata ujumbe ipasavyo. Hivyo, huamua kubadili msimbo ilikuleta uhusiano wao karibu. UM kiwakati hufanyika ghafla kwa sababu mzungumzaji hujipata tu ametumia lugha nyingine bila kupanga. Katika vipindi husika vya SK UM kiwakati ulidhihirika.

Kwenye kipindi cha *Tilyandit eng Katunisiet* (Uhusiano katika Ndoa), Rotich anasema hivi:

1. *Ngalen ingen o Winny ile makanye bikyok komwachi lagokwak tuguk che tinyegei akngono. Aegei sigik kou ne mengen lagok kole sikobit lakwa ni ku-practise' ngono.*

Winny, ninajua unafahamu kuwa watu wetu wanaogopa kuwaambia watoto wao mambo kuhusiana na ngono. Wazazi wanadhani kuwa watoto hawaelewi mtoto hupatikana kupitia njia ya ngono.

Neno ‘ngono’ katika mfano 1 ni la Kiswahili na limetumiwa kimuktadha kumaanisha kujamiiana. Wasemaji wa Kikalenjin wanaogopa sana kuyataja mambo kama hayo hadharani. Hii ndio maana Rotich ametumia neno la Kiingereza ili neno hilo lisionekane kuwa la aibu. Iwapo Rotich angetumia neno la Kinandi ‘*Keruiyo*’ (kujamiiana), lingeonekana kuwa hatari kwa sababu wasikilizaji ambao labda umri wao unapiku wa Rotich, wangeogopa kutoa mchango wao.

Sehemu ya mwisho ya mfano huo wa 1, inabeba kirai kitenzi ‘ni *Ku-practise* ngono’ ambacho kimeundwa kwa kuchanganya Kiswahili na kiingereza. Kirai kizima kinabeba maana ya kufanya zoezi hilo la ngono. Imeonekana vigumu kwa Rotich kusema sentensi lote kwa Kinandi kwa sababu kwake yeye na jamii yote husika, maneno kama hayo hayatajwi hadharani. UM basi umemsaidia msemaji Rotich kupitisha ujumbe wake lakini kwa kutunza heshima baina yake na hadhira.

Mfano mwingine ni katika mazungumzo katika kipindi cha *Koolokseet eng Katunisiet* (Mavazi na Ndoa). Winny anajaribu kuwatetea wasichana wa siku hizi akisema kuwa wakati unawalazimu kuvaa mavazi mafupi ili waonekane warembo. Kwa kumjibu, Rotich anatumia UM ifuatavyo:

2. *Winny, makikosyindosi eng yotok, kele wakat huu! Ngot kiyonji tibik kwai kunotok kou nee as chebo miaka zijazo!*

Winny, hatutakubaliana kwa hilo, unasema wakati huu! Iwapo binti zetu watakubaliwa wafanye hivyo, nani ajua watakavyofanya wa miaka zijazo!

Virai ‘wakati huu’ na ‘miaka zijazo’ ni vya Kiswahili. Virai hivyo vimetumiwa kimuktadha kulingana na mahitaji ya wakati. Rotich anatofautiana na maoni ya Winny kwa kuashiria alichosema Winny kuwa wasichana wa siku hizi wanajaribu kujirembesha kwa kuvaa mavazi vya aibu. Muktradha ndio umelazimu matumizi hayo ya UMili wazungumzaji waweze kuelewa vyema ujumbe unaotakiwa kupitishwa kwa wakati huo.

Katika kipindi cha *Korgtab yugoi ak ingamatisyek* (Wakwe katika Ndoa), Winny anatumia UM kitasfida ili kujali mahitaji ya uso wa hadhira yake. Ili kudhihirisha heshima kwa wasikilizaji anahepa matumizi ya lugha yake na anapendelea lugha ya Kiingereza katika kuhakikisha kuwa ujumbe wake umeeleweka licha ya kuzingatia upole. UMunampa msemaji nafasi nzuri ya kusema jambo analotaka bilakuhisi kuaibika. Anawatahadharisha mama wakwe kwa kusema:

3. *Mie konai mama nebo manong’otionyu kole kisicho agane kamenyu. Mat kobwat kole inegei ne kisigis amat kobwat kole werinyi inegei ne tinyei kamet. Machei konai kole process nebo conception ko kergei, no difference ee!*

Ni vyema mamake mume wangu ajue kuwa mimi pia nilizaliwa na mamangu. Asifikirie kuwa yeye pekee kazaa na asifikirie kuwa mwanae ndiye pekee ana mama. Anatakiwa kufahamu kuwa ule **mchakato** wa **kuchukuliwa mimba** ni sawa, **hamna tofauti!**

Kupitia mfano huo wa 3, UM unatumika katika hali ya kutaka kuzuia aibu miongoni mwa wahusika wa mazungumzo. Winny anahisi vyema anapotumia maneno ya lugha ya kiingereza badala ya yale ya lugha yake ili kuzuia aibu kati yake na wasikilizaji wake. Ni dhahiri kuwa anapotumia lugha nyingine, maneno ambayo yanaonekana ya aibu katika Kikalenjin yanatamkika kwa wepesi. Labda angesita kuyatamka maneno hayo katika lugha yake au kukwepa kabisa kuyataja au hata kutumia maelezo ambapo ujumbe uliotakiwa kupitishwa ungepotoshwa. Minu ya ubadilishaji msimbo kwa kuzingatia wakati na muktadha ni mbinu tosha ya kukabiliana na tishio kwa nyuso za wahusika wa mazungumzo.

UM Kimafumbo

UM wa kimafumbo hutumika wakati ambapo wazungumzaji hawataki mtu wa tatu aelewe wanachosema. Aidha, hutumiwa iwapo mtu asiyelewa lugha inayozungumzwa amefika. Pia, matumizi ya mafumbo husaidia katika kupitisha ujumbe usiokuwa wa moja kwa moja na ambao ungeweza kukwaza mawasiliano. Ni mbinu mojawapo ambayo hutumiwa na wasemaji ili hadhira ichukue nafasi ya kufasiri ujumbe husika. Hutumika tu iwapo wanaohusika wanaelewa matumizi yake. Hata hivyo, UM wa aina hii huzua mtafaruku wakati mwingine kwa kuwa sio kila mtu anayehusika katika mazungumzo yoyote yale anaelewa maana ya mafumbo yote.

UM kimafumbo ulibainika katika kipindi cha *Subseetab Kwonyik* (Ubakaji wa Wanawake). Winny anasema:

4. *Kegas iman ii Pasta? Ni kweli, nyani haoni kundule. Kegas komie ole kamwaita kastaindenyo? Kamwa komie kole kimakongen chepyosonotok kole kima ko kararan kaloksetab tibikyik. Kale kicham komwoe kila agobo lagokab jirani kobwatyin kole matinyei kasoro chechik, lakini mwisho msichana alibakwa nani!*

Umesikia kweli Pasta? **Ni kwelinyani haoni kundule.** Umesikia vizuri alivyosema msikilizaji wetu? Amesema vizuri kuwa huyo mama hakuwa anajua kuwa tabia na hali ya mavazi ya wanawe haikuwa ya kupendeza. Amesema kuwa huyo mama alikuwa na mazoea ya kuwasema vibaya binti za **jirani** akifikiria wake hawakuwa na **kasoro, lakini mwisho! Bintiye mmoja alibakwa.**

Katika mfano huo, baadhi ya maneno yaliyotumiwa kuwasilisha ujumbe ni ya Kiswahili. Mfano wa kwanza ni kirai **ni kweli** na methali **nyani haoni**

kundule ambayo ni kama fumbo. Baada ya msikilizaji huyo kutoa maoni yake kuwa akina mama ndio huchangia kubakwa kwa binti zao kwa kutowaonya dhidi ya kuvaa vibaya, Winny ‘analipuka’. Anafanya hivyo kwa kubadilisha msimbo ili kurahisisha mawasiliano na kujenga uhusiano mzuri kati yake na wasikilizaji. Anafanya hivyo kwa sababu ni vigumu kwake kutaja mambo hayo bayana. Msikilizaji atalazimika kufikiria sana ilia pate kuelewa maana ya kilichosemwa. Ni njia mojawapo ya kupitisha ujumbe unaokosoa bila kuzua mkwaruzano kati ya wazungumzaji na wasikilizaji. Sentensi ya mwisho katika mfano huo wa 2 ina maneno ya Kiswahili **jirani** na **kasoro**. Licha ya kuwa maneno hayo hayahusiani moja kwa moja na lugha ya kimaafumbo, yanazua wepesi fulani wa ujumbe kinyume na matumizi ya maneno ya Kinandi ambayo yangeonekana kupitisha ujumbe lakini kwa ugumu.

UM kimaafumbo unadhihirika pia katika kipindi cha *Tetetab Sigisiet* (Mpango wa Uzazi). Winny anamwambia Rotich kuwa, mara ya kwanza jamii ya Wakalenjin haikukumbatia mpango wa uzazi kwa sababu iliaminika kwamba mpango huo ulikusudiwa kusimamisha uzazi. Anaeleza kuwa imani ya wanajamii kuhusiana na dawa za kupanga uzazi ilikuwa kwamba watoto watakozaliwa baada ya kutumia mpango huo hawangeweza kuzaa. Rotich anakubaliana naye kwa kusema kuwa imani hiyo ilisababisha watu wengi kuzaa watoto wengi kupiku uwezo wao. Anatumia UM kwa njia ya mafumbo kwa kutaja idadi ya watoto wanaofuatana kama siku za juma akisema:

5. *Keer iman oh Winny kit ne kubit amu kayananotok bo buch o, kisich biik lagok che rubugei kou Monday, Tuesday, Wednesday, Thursday... ei, kibiit nyalilda kot!*

Winny, angalia kweli kilichotokea, kupitia kwa imani hiyo potovu, watu walizaa **watoto wanaofuatana kama Monday, Tuesday, Wednesday, Thursday...** ai, kulitokea shida!

Kama tujuavyo, *Monday, Tuesday, Wednesday na Thursday* ni siku za juma. Msikilizaji anapaswa kufikiria sana ili aweze kupata maana ya fumbo hilo ambalo limetumiwa kumaanisha watoto ambao wamezaliwa moja baada ya mwingine bila kuzingatia wakati mwafaka kati ya watoto hao. Kupitia fumbo hili, Rotich amefaulu kupitisha ujumbe wake bila kuwakera wasikilizaji wake.

Mfano mwingine wa matumizi ya UM wa kimaafumbo ni katika kipindi cha *Tuguk che Butei Katunisiet* (Vitu vinavyovunja ndoa), Rotich anatoa ushauri kwa wasikilizaji wote kuwa mpango wa kando unasababisha magonjwa ya zinaa au virusi vya UKIMWI. Anafanya hivyo kwa uangalifu sana ili asionekane kunyosha kidole kwa wasikilizaji. Kwa mfano anaposema:

6. *Kingen achek tugul kele ye kakoit AIDS, borto ne matinyei kerichoo, komugaksei kwalda chito tugul tugul che katabo lagok si keribe inendet. Of course ingen chitugul kora kole ye kagobek tuguk ak kwo chichotok kong'etu lagok ko kibananok che bonon.* Sotetunajua kuwa **UKIMWI** unapozuka, mtu anaweza kuuza maliambayo watoto wangerithi kwa ajili ya matibabu. **Kawaida**, kila mtu anafahamu pia kuwa baada ya kutumia kila kitu kwa matibabu na kuaga dunia, watoto watabaki mayatima, tena maskini.

Rotich anatumia maneno *AIDS*(UKIMWI) na *Of course*(kawaida) ambayo ni ya Kiingereza. Anabadilisha msimbo ili kukabiliana na tishio kwa uso wa hadhira. Mkakati huu wa kutumia ubadilishaji msimbo ni mbinu mojawapo ya upole chanya ambao unakusudia kujenga na kudumisha mahusiano ya wazungumaji. Hivyo basi, UM humsaidia mzungumzaji kujiepusha kutaja mambo ambayo yanaonekana kuvunja heshima baina yake na msikilizaji.

Changamoto za Ubadilishaji Msimbo

Licha ya urahisishaji wa mawasiliano, UM una matatizo yake. Kutokana na data yetu kutoka vipindi vya *SK*, ilibainika kuwa lugha zaidi ya moja zilitumika kuwasiliana. Lugha hizo ni pamoja na Kiingereza, Kiswahili na Kinandi. Mwelekezi na mwasilishaji wa vipindi husika walitumia Kiingereza na Kiswahili kutilia mkazo jambo au kuhepa kuhasiri nyuso za wasikilizaji. Iwapo neno lingeonekana kuwa tishio kwa uso wa msikilizaji, mzungumzaji angetumia lugha nyingine ili kupunguza makali ya usemi wake. UM huo ulionekana kurahisisha mawasiliano. Licha ya utenda kazi huo, UM ulionekana kuwa na matatizo mengi.

Kwanza, mwelekezi pamoja na mwasilishaji ni wasomi. Hata hivyo, wao ni wajuzi wa lugha ya Kinandi. Mashabiki wa vipindi vya *SK* ni mchanganyiko wa wasomi wa kiwango cha juu, kiwango cha wastani na kiwango cha chini. Zaidi ya hayo, kuna baadhi ya mashabiki ambao hawana kisomo kabisa. Kwa kupenyeza maneno ya Kiswahili na Kinandi, hao viongizi wa vipindi wana chukulizi kuwa wasikilizaji wote wanaelewa lugha hizo tatu vizuri. Ilidhihirika kuwa kuna baadhi ya wasikilizaji ambao hawakuelewa kilichomaanishwa. Hivyo basi, UM haukidhi mahitaji ya wasikilizaji wote wa vipindi vya *AK* kwa sababu hukwamiza mawasiliano.

Pili, UM huwafanya mashabiki kuhisi kuwa watumiaji wa lugha hizo wana maringo. Kwa mfano katika kipindi cha *Amu nee che ipchin murenik kotun kwonyik alak* (sababu za mwamume kuoa wake wengine), msikilizaji 'W' anadokeza kuwa wanawake waliosoma na kuolewa na wanaume wasio na kisomo, wanawaonyesha waume zao madharau. Anasema:

7. *Pasta, mi kwonyik che amu somanyotin kosir boisielwak kosasisiei. Ngap kong'alalji boiyot Kingereza ago melen is ile makasei Nandi. Notok amu nee si ngap kotunis chito kogeny*

Pasta, kunao wanawake ambao iwapo wamesoma kuliko waume zao huonyesha madharau. Wakati mwingine anaweza kumzungumzia mumewe kwa Kiingereza na sio kwamba haelewi Kinandi. Hiyo ndiyo sababu mtu anaweza kuamua kuoa tena

Kutokana na mfano huo, kuna dhihirisho kuwa baadhi ya watu huchukulia kuwa iwapo wazungumzaji wanaelewa lugha ya mama kisha mmoja wao akaamua kuchopeza lugha nyingine, kwao, huko kubadilisha lugha ni kiashiria cha maringo.

Tatu, matumizi ya UM wakati mwingine huaibisha. Iwapo mtu hakufika kiwango kizuri cha umilisi wa lugha nyingine kando na ya mama, kuna uwezekano wa kujiaibisha kwa kutumia lugha hiyo. Wengine wanaweza kutumia maneno ambayo hayafai katika sehemu fulani ya usemi na kuaibika wanapochekwa na wenzao, au kutamka neno tofauti na inavyotamkwa au hata kukanganyika kati ya maneno mawili. Mfano mzuri ni katika kipindi cha *Kalokseet eng Katunisiet* (Mavazi katika ndoa). Msikilizaji 'Y' analalama kuwa wanawake wanavaa mavazi yasiyosetiri miili yao kwa kusema:

8. *Koriryo, mochei ngap imwochini kwonyik ak tibiik konai kole makororon ngoroik che nwogen. Ngap ituiye lakwa ne kelach tugun che kikwong'e, ndagerin kogeer olin kou yo menginein amu aibu. Ang ye kakorusin kwong'et ipkosirto, koweek kabwotutik ibwat ile ngou yo 'familia' lakwanotok.*

Koriryo, wakati mwingine unatakiwa kuwaeleza wana wa kike kuwa mavazi mafupi si mazuri. Kuna wakati unaweza kukutana na binti aliyevaa kiajabu, na akuonapo hujifanya hakuoni na kuangalia kando. Baada ya kupigwa na butwaa, mawazo yako yanarudi na unanza kujiuliza iwapo sura uliyoona ni 'familia'.

Neno 'familia' limetumika vibaya katika mfano huo. 'Y' ametatanika baina ya neno la Kiingereza 'familiar' na neno 'familia' ambalo ni jina la aina ya unga wa uji. Jambo kama hili ni la kuaibisha na huwafanya mashabiki kuogopa kuchangia mjadala. Ni kwa msingi huu ndipo tunasema kuwa wale wanaotumia UM wanafaa kuwa waangalifu ili maneno yanayotumiwa yawe na maana inayokusudiwa.

Mwisho, wahusika wa mazungumzo wameonekana kutumia mbinu ya UM kama kuchukua sehemu ya tasfida. Wasemaji wa Kinandi hivi karibuni wamekuwa na mazoea ya kutumia UM badala ya tasfida za Kinandi, tasfida mojawapo ya mbinu zinazotumika kutekeleza mkakati wa upole chanya. Katika Kipindi cha *Tilyandit eng Katunisiet* (Mahusiano katika Ndoa), Pasta Rotich anaeleza kuwa akina mama wanatakiwa kuwa marafiki na binti zao. Anasema kuwa mama akimkaribia bintiye, kutoa maelekezo kwake kutakuwa rahisi. Anatumia mfano wa

wakati msichana ako katika hali yake ya hedhi na wazazi wanataka kujua sababu ya kutoenda shuleni. Pasta anasema kuwa ni vigumu kwa binti huyo kumweleza babake sababu kamili lakini kwa mamake itakuwa rahisi. Pasta anasema hivi:

9. *Igere ii Winny, nyamnyum mising eng tie kolenji kamet 'anyeshani' kosiir kwan. Ingen ile ma raisi yotok is!*

Winny, wajua, ni rahisi kwa msichana kumwambia mamake '**ninanyesha**' kulikokumwambia babake. Unajua hilo si rahisi.

Kupitia mfano huo wa tano, matumizi ya neno *anyeshani* (ninanyesha), yanaonyesha kuwa UM umechukua nafasi ya tasfida ya Kinandi *ami betusiek* (nina hedhi). Neno *anyeshani* limekopwa kutoka neno la Kiswahili 'ninanyesha'. Kwa hivyo UM unachangia kupotea kwa tasfida za Kinandi kwa sababu kusema katika Kiswahili kunaonekana rahisi kuliko Kinandi.

Mifano hiyo imeonyesha jinsi matumizi ya UM huweza kusababisha matatizo wakati wa mawasiliano. Ni muhimu kwa wahusika wa mazungumzo kuzingatia kiwango chao cha elimu na ya wenzao kabla ya kutumia mbinu ya UM. Kadhalika, mawasiliano yoyote yale licha ya kupunguza vitisho kwa uso wa msikilizaji yaweze kupitisha ujumbe uliokusudiwa.

Hitimisho

Katika makala haya tumechanganua matumizi ya UM kama mbinu mojawapo ya kutekeleza upole hasi katika vipindi vya *SK* katika idhaa ya Kass FM. Tumbainisha kuwa UM unatumika kupitisha ujumbe bila kutishia nyuso za wahusika wa mazungumzo. Tumeona kuwa vipindi vya *SK* huzungumzia mada zinazohitaji matumizi ya upole ili kukidhi mahitaji ya nyuso za wasikilizaji. Ni bayana kuwa, wahusika wa mazungumzo husika hupendelea UM badala ya tasfida za Kinandi. Hata hivyo, imedhihirika kuwa UM ni pigo kubwa kwa lugha ya Kinandi kwa sababu wazungumzaji wameikumbatia sana na hivyo kupunguza matumizi ya tasfida za Kinandi. Upunguzaji wa matumizi ya lugha yoyote ile unadhihirisha kupunguka kwa hadhi ya lugha husika. Changamoto hizo zimebainishwa wazi kupitia mifano kutokana na usemi wa wahusika.

Marejeleo

- Allan, K. & K. Burridge (2006). *Forbidden Words. Taboo and Consoring of Language*. New York: Cambridge University Press.
- Bailey, K. M. (2001). *Interactional Functions of Code Switching Among Dominican Americans*. From http://benjamins.com/catalog/prag,10.2.01_bai.
- Brown, P. & Levinson, S. (1987). *Politenes. Some Universals in Language Usage*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Brown, P. & Levinson, S. (1978). Universals in language use: politeness phenomena. Katika E. Goody (wahr). *Questions and Politeness* kur. 56-289. Cambridge: Cambridge University Press.
- Djoko, S. (2006). Code switching in Islamic Religion. Imepakuliwa kutoka <http://www.hum.nl/teun/cda.htm>.
- Grice, H.P. (1975). Logic and Conversation. Katika Peter Cole & Jerry Morgan (wahr.) *Syntax and Semantics*, Volume 3: Speech Acts, kur. 41-58. New York, NY: Academic Press.
- Kanana, F. E. (2003). Code Switching in Business Transactions. A case study of Pepertoire in Maasai Market in Nairobi Kenya. Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa.
- Mills, S. (2003). *Gender and Politeness*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Muthuri, D. (2000). Matumizi ya ubadilishaji msimbo baina ya wanafunzi wa wingi-lugha wa Chuo Kikuu cha Kenyatta. Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa
- Myres-Scotton, C. (1993). *Code Switching: Evidence from Africa*. New York: Oxford University Press.
- Ogechi, N. O. (2002). *Code Switching in Kenya, Evidence from Ekegusii, Kiswahili, English and Sheng*. Tasnifu ya uzamifu, Chuo Kikuu cha Humburg.
- Ogechi, N.O. (2006). Trilingual Codeswitching in Kenya – Evidence from Ekegusii, Kiswahili, English and Sheng. Tasnifu ya uzamifu ambayo haijachapishwa. Hamburg: University of Hamburg.
- Petríčková, I. (2012). *Politeness strategies in interview questions*. Tasnifu ya uzamili. http://is.muni.cz/th/325815/ff_b/Thesis.pdf
- Watts, R. (2003). *Politeness*. Cambridge: Cambridge University Press.

